# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. ANNA E. MGHWIRA, MKUU WA MKOA WA KILIMANJARO KATIKA UFUNGUZI WA KIKAO MAALUM CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) TAREHE 05 MACHI, 2021

- Ndugu Wajumbe wa Kamati ya Usalama ya Mkoa;
- Ndugu Katibu Tawala wa Mkoa;
- Mheshimiwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro;
- Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya;
- Ndugu Waheshimiwa Wabunge;
- Ndugu Mstahiki Meya;
- Ndugu Wenyeviti wa Halmashauri;
- Ndugu Wakuu wa Taasisi mbalimbali;
- Ndugu Wana-Habari;
- Mabibi na Mabwana:

**Ndugu Wajumbe;**
Awali ya yote napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mungu kutuleta pamoja katika kikao hiki. Pili, kuwakaribisha wajumbe wote katika kikao hiki maalum cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) kwa ajili ya kupitisha makisio ya Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022.

Napenda kuwakaribisha wale wote ambao ni mara yao ya kwanza kushiriki katika vikao vya RCC hapa Mkoani kwetu.

Pia nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa katika kutekeleza majukumu makubwa tuliyonayo hivi sasa. Tumepata ushirikiano mkubwa katika kuwapokea wanafunzi wa darasa la kwanza na vile vile kuhakikisha wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wameweza kuanza masomo yao vizuri.

Pia nasisitiza matumizi ya takwimu sahihi katika maandalizi ya bajeti ili kupunguza changamoto mbalimbali zinazokabili sekta ya elimu.

Aidha, kuendelea kupima na kuandaa hatimiliki kwa maeneo ya umma ikiwemo shule za msingi, sekondari, zahanati na vituo vya afya.

**Ndugu Wajumbe;**
Napenda sote tuelewe kuwa mojawapo ya majukumu ya Halmashauri zetu ni kutoa huduma kwa wananchi pamoja na kusimamia masuala ya maendeleo. Utekelezaji wa majukumu hayo unalenga katika kutekeleza vipaumbele vya wananchi ambavyo vinahitaji fedha kutoka kwa wadau mbalimbali mathalani serikali kuu, wadau wa maendeleo na vyanzo vya mapato vya Halmashauri zetu.

Mwaka wa fedha 2020/21, Halmashauri zetu zinategemea kutumia jumla ya shilingi **256 bilioni** kwa ajili ya mishahara – **181.88 bilioni,** matumizi mengineyo **25.695 bilioni** na miradi ya maendeleo **48.377 bilioni.**

Kati ya fedha hizo, shilingi **7.4 bilioni** pekee zinatokana na makusanyo ya ndani ya Halmashauri (Own Source) sawa na asilimia **19%** ya bajeti idhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. Kwa mantiki hiyo, Halmashauri zetu zinachangia kiasi kidogo sana na mara nyingi malengo yanayowekwa kila mwaka hayafikiwi; hivyo ni wajibu wa kila Halmashauri kuongeza ubunifu wa vyanzo na mbinu za ukusanyaji wa mapato ili kufikia malengo ya ukusanya na utoaji wa huduma bora kwa jamii.

Kwa mfano: hadi mwezi Januari, 2021, Halmashauri zimekusanya shilingi **11.22 bilioni** sawa na 48% tu ya lengo la ukusanyaji kwa mwaka wa fedha **2020/2021.**

Aidha, tunashukuru, Serikali imeturejeshea chanzo cha makusanyo yatokanayo na nyumba ***(Property Tax),*** hivyo kuwa na chanzo kingine cha uhakika cha mapato. Ni imani yangu kwamba, tutaongeza juhudi za ukusanyaji kutoka kwenye chanzo hicho ikiwa ni pamoja na kuwa na takwimu sahihi za nyumba zote zinazotakiwa kulipiwa kodi katika Mkoa wa Kilimanjaro.

Kutokana na takwimu hizo ni wazi kuwa hali ya makusanyo yetu ya ndani si nzuri. Mapato ya Halmashauri zetu yamekuwa yakitegemea kwa kiasi kikubwa fedha kutoka Serikali Kuu. Hii ni kiashiria kwamba kwa siku za usoni Halmashauri zitashindwa kutoa huduma kwa wananchi kama hatutaongeza ubunifu na kushirikiana kuongeza mapato yetu ya ndani. Ni lazima Halmashauri zetu zibuni vyanzo vipya vya mapato. Sheria ya makusanyo ya kodi ya huduma ***(Service Levy)*** isimamiwe ipasavyo na Halmashauri zote. Hiki ni chanzo kikubwa cha mapato.

Aidha, nawakumbusha kuendelea kutoa/kurejesha asilimia itokanayo na makusanyo ya ndani kwa vijiji/mitaa ili jamii iendelee kuona umuhimu wa kodi zinazokusanywa.

Kwa kipindi cha mwaka 2020/21 makisio ya 10% kwa ajli ya mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemevu ni Tsh.**1.56** bilioni ambapo kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2020 Halmashauri zilitakiwa ziwe zimeshatoa kiasi cha Tsh. **572 milioni** kulingana na makusanyo ya kipindi hicho. Takwimu zinaonyesha jumla ya shilingi **298 milioni** tu sawa na **52%** ndizo zilizotolewa kwa kipindi tajwa. Aidha nazitaka Halmashauri uongeza kasi ya utoaji wa fedha hizo kwa wakati kwa kuzingatia makusanyo ya kipindi husika.

Napenda nitoe wito kwa Kamati zote za Fedha na Viongozi wa Halmashauri kuhakikisha kuwa na usimamizi mzuri katika mgawanyo wa mapato ya ndani kutegemeana na sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Nielekeze pia ofisi ya Katibu Tawala Mkoa – kujipanga vizuri katika kitengo cha Uratibu – tupate watu wenye uwezo na utashi wa kuzisaidia Halmashauri zetu kufikia malengo ya kazi zetu. Vivyo hivyo kitengo cha Serikali za Mitaa. Hivi ni vitengo muhimu vinavyohitaji ziada ya utaalam na utashi halisi katika kuinua kazi zetu.

**Ndugu Wajumbe;**
Katika utekelezaji wa dhana ya Utawala Bora bado kuna mapungufu na tuna kazi kubwa ya kufanya ili kuweza kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora kwa haraka zaidi na kwa wakati. Viongozi na wataalamu wote tushirikiane katika kuhakikisha kero na malalamiko ya wananchi yanashughulikiwa ipasavyo. Nimefurahi kuona kuwa, **kila Ofisi ya Serikali imefungua Dawati la Kusikiliza Kero/Malalamiko ya Wananchi.** Haya ni maelekezo ya Serikali, hatuna budi kuyasimamia kwa nguvu zetu zote. Nimtake Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa kuhakikisha tuna watu waadilifu, weledi na waelewa sana katika kitengo hicho.

Kwa kipindi hiki ushahidi unaonyesha kuwa, bado tunahitaji kuboresha namna ya kuwasikiliza na kutatua kero za wananchi. Bado tunaendelea kushuhudia wananchi wakiwasilisha kero na malalamiko yao katika Ofisi zetu Mkoani na hata ngazi za juu. Natoa wito kwa viongozi na wataalam wote tushirikiane katika kutatua kero na malalamiko ya wananchi kwa uharaka zaidi katika maeneo yetu. Taifa lina maeneo ya utawala toka ngazi ya msingi kabisa ya Kitongoji, Kijiji na Mtaa.

**Ndugu Wajumbe;**
Katika msimu wa kilimo 2019/2020; chakula kilichozalishwa ni **tani 1,644,008** za mazao ya chakula na biashara katika hekta **339,435** zilizolimwa kati ya malengo ya kuzalisha tani **1,702,160** katika hekta **353,546.** Chakula halisi kilichozalishwa ni tani tani **619,426** za wanga na tani **76,165** za protini, wakati mahitaji yetu ya chakula kimkoa ni tani **453,670** za wanga na tani **45,367** za protini za mikunde. Mahitaji haya ni kwa makadirio ya watu **1,906,978** kwa mujibu wa sensa ya maoteo. Kwa takwimu hizi inaonesha kwamba kwa mwaka huu kuna ziada ya tani **165,756** za wanga na tani **30,798** za protini au utomwili. Kwa sasa hatuna upungufu wa chakula kwa maana ya upatikanaji wa vyakula masokoni unaridhisha na bei ni ya wastani; hata hivyo napenda kutoa wito kwa viongozi wote kuelimisha wananchi kuhifadhi na kusimamia vizuri matumizi ya chakula kilichopo.

Aidha, msimu wa kilimo cha masika 2020/2021 ambacho ndicho kilimo kikubwa unakaribia na maandalizi ya yameanza. Natoa rai kwa viongozi na watalaamu kusimamia na kuelekeza wananchi kufanya maandalizi ya mashamba kwa wakati na kuzingatia ushauri wa kitaalamu. Pia viongozi katika ngazi zote tushirikiane kusimamia kikamilifu matumizi sahihi ya pembejeo za ruzuku inayotolewa na Serikali ili ilete tija.

**Ndugu Wajumbe;**
Tunazo changamoto nyingi zinazokabili Halmashauri zetu. Hapa nataja baadhi ya changamoto hizo ili tuweze kukumbushana, kuzijadili na kuona namna ya kuzitatua kwa kutumia mapendekezo ya bajeti ambayo tutaipitisha hivi punde katika kikao hiki.

- Uchache wa vyanzo vya makusanyo (mapato katika mamlaka ya Serikali za Mitaa). Natoa wito kuendelea kufanyia kazi vianzio vipya vya mapato katika sekta ya uvuvi na ufugaji.

- Fedha toka Serikali Kuu kuchelewa kupatikana na hivyo utekelezaji wa miradi/shughuli kutofanyika kwa wakati kama ilivyokusudiwa.

Kutokana na changamoto hizo, napenda nitoe maelekezo yafuatayo:-

- Halmashauri ziongeze ubunifu katika kutafuta vyanzo vipya vya mapato ambavyo ni vya uhakika na vya kudumu, pamoja na kuhuisha tozo za kodi kwa vyanzo vilivyopo ili vilingane na bei ya soko;

- Baadhi ya vyanzo katika Halmashauri zetu ni pamoja na ujenzi wa mialo Bwawa la Nyumba ya Mungu – wilayani Mwanga, ufufuaji wa kiuchumi Bwawa/Ziwa Jipe; Uanzishaji na usimamiaji wa ranchi za vijiji katika Halmashauri zote; na kuimarisha biashara ya mazao ya mifugo.
- Kipekee kuna suala la Ushirika na Usimamizi wa vyama hivi kwa namna inayoweza kuinua mapato ya Halmashauri.
- Halmashauri zote zihakikishe zinaendelea kutenga asilimia **10** kwa ajili ya mfuko wa akina mama, vijana na watu wenye ulemavu kadri ya makusanyo ya ndani. Ukikusanya shilingi **100** tenga shilingi **10** kwa ajili hiyo;
- Halmashauri zote zitenge asilimia 60/asimilia 40 kwa mapato ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Haya ni maagizo ya Bunge na kwenye mwongozo wa bajeti 2021/2022 jambo hili limesisitizwa tena;

- Watoa maamuzi katika mamlaka zetu wahakikishe wanajifunza kwa makini na kuelewa sheria, taratibu na kanuni na sera mbalimbali ili ziweze kuwasaidia kufanya maamuzi ambayo hayawezi kuleta athari ya kuwepo matumizi mabaya ya madaraka;
- Kuhakikisha Taasisi sote za umma zikiwemo halmashauri zinatumia mfumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa kodi, ada, ushuru na tozo ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato;
- Kulipa madeni yaliyopo katika Halmashauri na kuzuia ongezeko la madeni.

Mwisho, baada ya kusema hayo, natangaza rasmi kuwa, kikao kimefunguliwa.  Nawakaribisha na kuwatakia mjadala mwema kwa maendeleao ya Mkoa wetu.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza!**